# HOTUBA YA WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**Utangulizi**

1. ***Mheshimiwa Spika***, Naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) kwa Mwaka 2025/26. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/25 na lijadili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka 2025/26.

**Shukrani na Pongezi**

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa **19** wa Bunge la **12** ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili bajeti ya Serikali. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tarehe 8 Disemba, 2024. Vilevile, napenda kumshukuru kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi ya kusimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa juhudi, maarifa na uadilifu ili kuwezesha nchi kufikia adhma ya kuwa na Uchumi wa Kidijitali.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka minne **(4)** tangu aingie madarakani. Katika kipindi cha uongozi wake Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepata mafanikio makubwa ikiwemo; Kuanza ujenzi wa minara **758** katika kata **713** kupitia mradi wa Tanzania Kidijitali; Kuanza ujenzi wa minara **636** nchini kupitia mradi wa Mawasiliano Vijijini; Kufikisha huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye Wilaya **109** kutoka Wilaya **36** nchini; Kufikisha Mkongo wa Taifa katika nchi ya Msumbiji

na Kuanza taratibu za ufikishwaji wa Mkongo katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; Kuongeza huduma ya mtandao wenye kasi kwenye maeneo ya watu *(Population Coverage)* kutoka **asilimia 40** hadi **asilimia 91**; Kuimarisha upatikanaji wa intaneti nchini kwa kuongeza mkongo mmoja wa baharini wa 2Afrika; Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na mikongo ya baharini iliyopo Mombasa Kenya kupitia mpaka wa Horohoro mkoani Tanga; Kufanyika kwa Operesheni Anwani za Makazi mwaka 2022 na Kuandaa Mkakati wa miaka kumi (2024 – 2034) wa Uchumi wa Kidijitali. Wizara inatambua umuhimu na matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kufikisha huduma za Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa wananchi kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Aidha, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuongoza vyema, kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar pamoja na kuendelea kudumisha na kuuenzi muungano wetu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** Niwapongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru kwa maelekezo na ushauri wao wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Sekta hii muhimu kwa Maendeleo ya Taifa letu. Aidha, ninampongeza Mhe. Waziri Mkuu kwa Hotuba yake ya Bajeti ambayo imetoa utekelezaji wa malengo ya Serikali kwa mwaka 2024/25 pamoja na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2025/26. Napenda kuahidi kuwa, Wizara itayafanyia kazi masuala yote yanayohusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yaliyoainishwa katika hotuba hiyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muugano wa Tanzania kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kazi wanayoifanya ya kukusaidia kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa

kusimamia shughuli za Bunge kwa maslahi ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushirikiano wao kwangu na Wizara kwa ujumla katika kuhakikisha malengo ya sekta yanafikiwa. Aidha, ninaishukuru Kamati kwa kujadili na kupitisha kwa kauli moja Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68, kwa Mwaka 2025/26. Ni ukweli usiopingika Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Maelekezo na ushauri wao kwa Wizara umezingatiwa, Wizara inaahidi kuendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati katika mwaka 2025/26 kwa maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tunasema **KAZI IENDELEE.** Vilevile, napenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu hususan wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali zinazohusu Wizara. Wizara, itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufanya uteuzi wa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi (Mb.). Kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ninampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa katika nafasi hiyo.

**Salamu za Pole**

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Familia na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Cleopa David Msuya, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni kwa tiketi ya CCM na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina

**Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

10. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina majukumu ya Kuandaa, kusimamia na

kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (TEHAMA), Posta na Mawasiliano ya Simu; Kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Sera, Mipango na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali kwa wananchi; Kufanya tafiti za maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA; Kuendeleza wataalam wa TEHAMA; Kuanzisha na kusimamia Postikodi; Kusimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; Kusimamia ulinzi na usalama wa mtandao; Kuboresha na kuendeleza utendaji wa rasilimali watu ndani ya Wizara na Kusimamia taasisi, programu na miradi ndani ya Wizara.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inasimamia Taasisi **Saba (7)** ambazo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL); Shirika la Posta Tanzania (TPC); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); Tume ya TEHAMA (ICTC); Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC).

**Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2023, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imekua kwa **asilimia 7.6** mwaka 2023 ikilinganishwa na **asilimia 7.4** mwaka 2022. Aidha, Sekta hii imechangia **asilimia 1.4** mwaka 2023 kwenye pato la Taifa ikilinganishwa na **asilimia 1.5** mwaka 2022. Hata hivyo, takwimu hizi zinaonesha kuwa mchango wa Sekta ni mdogo ikilinganishwa na uhalisia**.**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni mhimili na kichocheo kikuu cha uchumi, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara kwa kushirikiana na wadau wote muhimu wa ukokotoaji wa Hesabu za Taifa (System of National Accounts) ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), inatarajia kuanzisha Akaunti Maalum ya Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy Satellite Account – DESA) ili kuongeza wigo wa upimaji wa mchango wa sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa lengo la kutambua kwa usahihi mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa**.**

**Hali ya Upatikanaji wa Mawasiliano Nchini**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kukua, takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **milioni 73.5** Aprili, 2024 hadi laini **milioni 90.4** Aprili, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 22.9**. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka **milioni 37.3** Aprili, 2024 hadi **milioni 49.3** Aprili, 2025 sawa na ongezeko

la **asilimia 32.3.** Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka **milioni 53.7** Aprili, 2024 hadi **Milioni 66.5** Aprili, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 23.9.** Aidha, Idadi ya Watoa Huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano imefikia **38** Aprili 2025 ikilinganishwa na watoa huduma **27** Aprili, 2024 hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 40.7**. Watoa huduma za ziada (Application Services and Value-Added Services) wamefikia **136** ikilinganishwa na watoa huduma **122** mwezi Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia **11.5.**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo huu unaashiria kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano na teknolojia ya habari katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma za mawasiliano. Hii imewezesha wananchi kufikiwa na huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi kidijitali kama vile huduma za Kifedha, afya kwa urahisi na kwa haraka. Vilevile, ongezeko la huduma za Mawasiliano limechochea ukuaji wa uchumi wa watu na taifa kwa ujumla hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imejikita katika kujenga uchumi wa kidijitali.

**Hatua iliyofikiwa ya Utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidigitali**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka kumi (2024 – 2034). Mkakati huu unaweka misingi ya kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA ambapo utekelezaji wa Mkakati huu utawezesha kukuza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma Serikalini. Ili kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huu, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutafsiri Mkakati kwa lugha ya Kiswahili ili kuwezesha wananchi wote kushiriki katika utekelezaji wa Mkakati pamoja na Kutoa elimu kwenye Taasisi za Serikali na binafsi kupitia mitandao ya kijamii, redio na televisheni.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Uwepo wa miundombinu ya mawasiliano nchini ni chachu ya kuwezesha Serikali kufikia Uchumi wa Kidijitali. Katika hili Serikali chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa kwenye Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ikiwemo kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hadi sasa Wilaya **109** kati ya **139** zimeunganishwa, Ujenzi wa Miundombinu ya mkongo wa baharini na nchi kavu inayounganisha Tanzania na Mataifa mengine duniani, Ujenzi wa Minara **758** na kuanza ujenzi wa minara **636** kote nchini na kuongezea uwezo minara **304** toka teknolojia ya 2G kwenda 2G/3G au 4G ili kuongeza matumizi ya intaneti. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2025 Miundombinu ya brodibendi inayotoa huduma za

intaneti kiganjani kwenye maeneo ya watu imefikia asilimia **91** kutoka asilimia **80** Aprili, 2024. Pia, Serikali inaendelea na mradi wa kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo ya wazi hamsini **(50)** yanayotumiwa na wananchi katika shughuli zao za kila siku ili kuongeza na kuhamasisha matumizi ya mtandao wa intaneti nchini. Maeneo hayo ni pamoja na masoko, stendi za mabasi makubwa na madogo na vituo vya mwendokasi.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufikia adhma ya kuwa na Uchumi wa Kidijitali, Wizara yangu imeratibu ujenzi wa mifumo mitano **(5)** ya kitaifa: Mfumo wa ubadilishanaji taarifa (Jamii X-change na ZanXchange) ambayo inasimamiwa na Mamlaka za Utambulisho (NIDA na ZCSRA); Mfumo wa utambuzi kidijitali (Jamii Namba), mfumo wa Utambuzi wa wateja (e-KYC), Mfumo wa malipo ya kidijitali (Jamii Pay) na mfumo wa usajili na uwezeshaji wa Wadau wa ikolojia ya tafiti na bunifu za TEHAMA ikiwemo kampuni changa (safari hunt). Aidha, kwa upande wa kisekta, Wizara imeratibu uboreshaji wa mifumo ya utambuzi na usajili kwenye taasisi za RITA na NECTA. Ujenzi wa mifumo hii inarahishisha utoaji wa huduma za Serikali na wananchi kwa ujumla.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kufikia lengo la Mheshimiwa Rais la nchi kuwa na Satelaiti yake, Wizara imeanza taratibu za kuridhia Mikataba miwili **(2)** ya anga za juu ambayo ni Mkataba wa Kanuni zinazosimamia Shughuli za Mataifa Katika Utafiti/ Uchunguzi na matumizi ya Anga za Juu wa mwaka, 1967 na Mkataba wa Usajili wa vifaa/Vyombo vilivyorushwa katika Anga za Juu wa Mwaka, 1975. Kukamilika kuridhiwa kwa Mikataba tajwa kutatoa fursa kwa Wizara kuandaa Sera ya Anga za Juu na mkakati wake wa utekelezaji ambao utawezesha kuimarisha teknolojia ya anga za juu na satelaiti.

**Gharama za Mawasiliano ya Simu**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa bei ya dakika ndani ya mtandao bila kifurushi (Shilingi/dakika) zimeendelea kubakia wastani wa **Shilingi 26** kutoka mwezi Juni, 2024 hadi kufika Aprili, 2025, wakati bei ya dakika nje ya mtandao bila kifurushi imeendelea kubakia wastani wa **Shilingi 28.0** kutoka mwezi Juni, 2024 hadi kufikia Aprili, 2025. Mwenendo wa gharama za rejareja za data bila kifurushi na kwenye kifurushi zimeendelea kupungua. Aidha katika robo ya mwaka inayoishia Machi, 2025, gharama za data ndani ya kifurushi zimeshuka kwa kiasi kidogo na kufikia wastani wa **Shilingi 2.12** kwa *Megabyte* Aprili, 2025 ikilinganishwa na Shilingi **2.16** kwa *Megabyte* Juni, 2024. Usajili wa vikoa umeongezeka kufikia **33,494** Aprili, 2025 ukilinganisha na vikoa **30,090** vilivyosajiliwa kipindi kilichoishia Juni, 2024. Hili ni ongezeko la vikoa

**3,404** sawa na **asilimia 11.3.**

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2024/25**

**Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 100.7** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida. Hadi kufikia Aprili, 2025 Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 56.2** sawa na **asilimia 55.8** ya lengo.

**Bajeti iliyoidhinishwa**

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara iliidhinishiwa kutumia **Shilingi bilioni 180.9.** Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 38.9** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 24.99** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi bilioni 13.9** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Shilingi bilioni 142.0** iliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo **Shilingi bilioni 116.4** ni fedha za ndani na **Shilingi bilion**i **25.6** ni fedha za nje.

**Fedha zilizopokelewa na Wizara**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 161.6** sawa na **asilimia 89.3** ya **Shilingi bilioni 180.9** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka 2024/25. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **bilioni 13.4** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 11.1** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 137.1** ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha za miradi ya maendeleo inajumuisha **Shilingi bilioni 78.9** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 58.2** ni fedha za nje.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25**

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

   i. Kuandaa Rasimu za Mapendekezo ya kutunga Sera mpya ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2025 na kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali kwa ajili

ya kuridhiwa;

ii. Kufanya mapitio ya Kanuni saba (7) za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambazo ni Kanuni za Maudhui Mtandaoni, Kanuni za Ubora wa Huduma za Mawasiliano, Kanuni za Leseni, Kanuni za Posta, Kanuni za Timu ya Uitikiaji wa Majanga ya Mtandao, Kanuni za Usajili wa Laini za Simu na Kanuni ya Viwango vya Ubora wa Vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki na usimamizi wa taka zitokanazo na vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki;

iii. Kuunganisha mifumo **898** ya kutolea huduma. Kati ya mifumo hiyo mifumo **514** ni ya Serikali na mifumo **384** ni ya Sekta binafsi;

iv. Kusambaza na kusimika vifaa vya mkutano mtandao (*video conference)* kwenye Halmashauri **100**.

v. Kukamilisha ujenzi wa minara **482** kati ya **758** iliyopangwa kujengwa katika Kata **713** sawa na **asilimia 63.6** kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Aidha, minara **304** kati ya **304** iliyopangwa imeongezewa nguvu sawa na **asilimia 100;**

vi. Kuanza ujenzi wa Minara ya simu na redio **636** ambapo hadi Aprili, 2025 minara ya simu **141** imekamilika kati ya hiyo minara **68** inatoa huduma za mawasiliano;

vii. Kukamilika kwa usimikaji wa vifaa (Active installations) katika maeneo 25 kati ya maeneo 621. Aidha, usimikaji wa vifaa (mitambo) ya Core Network (DataCenter) katika vituo vya TTCL Dar es Salaam Telephone House na TTCL Dodoma Telephone House umekamilika;

viii. Kuhakiki anwani za makazi katika Halmashauri **13** (Tanzania Bara 11 na Zanzibar 2) hivyo, kufanya jumla ya Halmashauri **41** nchini kufanyiwa uhakiki;

ix. Kuunganisha Mfumo wa NaPA na mifumo mingine **13** ya kutolea huduma. Aidha, Mifumo mingine saba **(07)** ipo katika hatua mbalimbali za uunganishaji;

x. Kuanza taratibu za ununuzi wa vishikwambi **3,482** kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za anwani za Makazi;

xi. Kuunda moduli mbili (2) za Mfumo wa NaPA kwenye vivutio vya utalii na kutoa barua ya utambulisho kidijitali;

xii. Kukusanya taarifa za Anwani za Makazi za huduma na vituo vya utalii katika hifadhi 24. Kati ya hizo hifadhi tatu (3) ni za Ngorongoro na 21

TANAPA;

xiii. Kufanya maboresho ya mfumo wa NaPA ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa huduma za Anwani za Makazi kupitia USSD code;

xiv. Kujenga uwezo kwa wataalam na watendaji wa Serikali za Mitaa 8,010 kati ya 31,465;

xv. Kutoa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi **30** wa Serikali katika vyuo vikuu mbalimbali nchini Uingereza, Ujerumani, Malaysia, Uturuki na Sweden. Aidha, Watumishi **450** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya usalama mtandao, *Software Development, System Administration, Artificial Intelligence na Block Chain* kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali;

xvi. Kuratibu ujenzi wa mifumo mitano (5) ya kitaifa: Mfumo wa ubadilishanaji taarifa (Jamii X-change na ZanXchange) ambayo inasimamiwa na Mamlaka za Utambulisho (NIDA na ZCSRA); Mfumo wa utambuzi kidijitali (Jamii Namba), mfumo wa Utambuzi wa wateja (e-KYC), Mfumo wa malipo ya kidijitali (Jamii Pay) na mfumo wa usajili na uwezeshaji wa Wadau wa ikolojia ya tafiti na bunifu za TEHAMA ikiwemo kampuni changa (safari hunt). Aidha, kwa upande wa kisekta, Wizara imeratibu uboreshaji wa mifumo ya utambuzi na usajili kwenye taasisi za RITA na NECTA;

*xvii.* Kuandaa Miongozo mitano **(5)** ya usimamizi wa TEHAMA ambayo ni: Mwongozo Bora wa matumizi ya TEHAMA, Mwongozo wa TEHAMA kwenye makundi Anuai, *Enterprise Architecture Framework, Interoperability na Standardization Framework* na *Digital Public Infrastructure Tanzania technology Stack;*

xviii. Kukamilisha ujenzi wa Kilomita **3,621** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kati ya Kilomita **4,442** sawa na **asilimia 82**. Utekelezaji huu, umewezesha kujengwa kwa jumla ya Kilomita **13,820** kati ya kilomita **16,280** tangu mradi kuanza**.** Aidha, ujenzi wa vituo vyote **111** vya kutolea huduma za Mkongo umekamilika kwa **asilimia 100.**

xix. Kukamilisha ufikishwaji wa Mkongo wa Mawasiliano kwenye Wilaya **10** za Bahi (Dodoma), Kilindi (Tanga), Chemba (Dodoma), Kilosa (Morogoro), Kwimba (Mwanza), Siha (Kilimanjaro), Mpwapwa (Dodoma), Mlele (Katavi), Malinyi (Morogoro), na Kalambo (Rukwa) hivyo kufanya Wilaya **109** kati ya **139** sawa na **asilimia 78** kufikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

xx. Kukamilisha ufikishaji wa Mkongo wa Taifa Mombasa (Kenya) kupitia kituo

cha Horohoro - Tanga;

xxi. Kukamilisha uunganishaji vituo **59** vya RUWASA kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

xxii. Kuunganisha maeneo manne (4) na huduma ya Wi-Fi kwenye Vituo vya Treni ya Mwendokasi (SGR) vya Dar es Salaam, Morogoro, na Dodoma pamoja na uwanja wa Taifa wa Benjamini Mkapa hivyo kufanya maeneo yaliyounganishwa kufikia **10**;

xxiii. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Mahiri cha TEHAMA (DTI) Nala - Dodoma;

xxiv. Kuhuisha Mfumo wa takwimu za makosa ya mtandao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

xxv. Kuzindua Kampeni ya Usalama Mtandaoni **"SITAPELIKI"** ili kupunguza utapeli na ulaghai Mtandaoni;

xxvi. Kutoa leseni za mawasiliano **2,886** kati ya hizo, **529** ni leseni za rasilimali namba, **1,850** ni leseni ndogondogo na **487** ni leseni kubwa (individual licences);

xxvii. Kubaini na kuzifungia laini za simu **47,728** pamoja na Nambari ya Kitambulisho cha Taifa **39,028** ambazo zimehusika katika uhalifu;

xxviii. Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mikongo (Fibers) na miundombinu ya watoa huduma za mawasiliano katika Mikoa **30** Tanzania Bara na Visiwani;

xxix. Kufanya ukaguzi wa vifaa vya kielektroniki **678** kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi. Kati ya vifaa hivyo, vifaa **278** vilikidhi vigezo na kuidhinishwa kwa matumizi. Aidha, uhakiki wa vifaa **400** unaendelea;

xxx. Kuimarisha Ushiriki wa Tanzania Kikanda na Kimataifa ambapo Wizara imeshiriki kwenye Baraza la Uongozi la ITU; Mkutano wa ITU-T wa WTSA-2024 nchini India; Kongamano la Kimataifa la Anga za Juu lililofanyika Jijini Milan Italy; Mkutano wa Baraza la Uendeshaji wa Posta (POC) na Baraza la Utawala (CA) la UPU;

xxxi. Kusainiwa kwa mkataba wa kukabidhi miundombunu ya Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano kwa Serikali ambapo hadi sasa jumla ya kilometa **336** kati ya **2,020** zimekabidhiwa;

xxxii. Kuanza ujenzi wa vituo nane (8) vya kikanda vya ubunifu wa TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Tanga, Lindi, Dodoma, Pwani, Mtwara na Mjini Magharibi;

xxxiii. Kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi **2,829**;

xxxiv. Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Wizara Mtumba, Jijini Dodoma ambapo hadi Aprili, 2025 ujenzi umefikia **asilimia 95.**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu mengine ya Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yameainishwa kwenye Ukurasa wa 15 hadi 38 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

**MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26**

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na Taasisi zake zimeandaa mpango wake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa wakati wa kuhutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Ahadi na Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Dira ya Taifa ya Maendeleo; na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26. Aidha, Wizara, imezingatia Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2025/26.

**Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka 2025/26**

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2025/26 Wizara itajikita katika utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo;

i. **Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:** kwa Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 – 2034; Kukamilisha marekebisho ya Sera ya Posta ya mwaka 2003; Kukamilisha utungwaji wa Sera Mpya ya TEHAMA ya mwaka 2025; Kuanza taratibu za utungwaji wa Sera ya Anga za Juu na Sera ya Kampuni Changa *(Start-up Policy)*; Kukamilisha taratibu za uridhiwaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014, Kukamilisha taratibu za uridhiwaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Anga la Juu, na Kuanza taratibu za utungwaji wa Sheria ya Anwani za Makazi na Sheria ya TEHAMA.

ii. **Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini**; kwa kukamilisha ujenzi wa Minara **758** kwenye Kata **713** nchini, Kuendelea na ujenzi wa minara **636** nchini kupitia mradi wa mawasiliano vijijini na Kuendelea kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya Mawasiliano maeneo ya mipakani.

iii. **Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao Nchini**; kwa Kuhakiki taarifa za Anwani za Makazi katika Halmashauri 28 nchini na Kusimamia uundaji wa mfumo wa kidigitali

utakaowezesha biashara Mtandao (e-Commerce).

iv. **Kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali**; kwa Kuunganisha Wilaya **11** nchini na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Nchi jirani ya DRC kupitia Ziwa Tanganyika, na Kuunganisha wateja 90,000 na huduma za "Faiba Mlangoni Kwako" (Broadband) kufikia Juni 2026.

v. **Kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao;** kwa Kujenga uelewa kwa wananchi juu ya Ulinzi wa data na Faragha zao na jinsi ya kukabiliana na matukio ya Utapeli na wizi mtandaoni; Kuwezesha upatikanaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa matukio na makosa ya mtandao nchini; Kuongeza uwezo kitengo cha uchunguzi wa kidijiti kwa Jeshi la Polisi katika ofisi ya makao makuu Katika kanda ya Mbeya na Mwanza; Kutoa Elimu juu ya Miongozo ya Miundombinu Muhimu ya TEHAMA na kuimarisha Ulinzi wa miundombinu hiyo.

vi. **Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa (Startups)**; Kusimamia uanzishwaji wa Vyuo viwili (2) vya TEHAMA Nala - Dodoma na Buhigwe – Kigoma; Kuwezesha uazishwaji wa vituo vinne (4) vya kukuza bunifu za TEHAMA kwa ngazi ya Wilaya; Kuwezesha uazishwaji wa vituo viwili (2) vinavyotembea vya kupata taarifa za TEHAMA (Mobile Access Centers); na Kusimamia utekelezaji wa vituo nane (8) vya ubunifu wa kidijitali katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam, Tanga, Lindi na Zanzibar.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mipango mingine ya Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imefafanuliwa katika Ukurasa wa 39 hadi 54 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

**SHUKURANI**

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kusimamia vema utekelezaji wa majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa **Maryprisca Winfred Mahundi (Mb.),** Naibu Waziri; **Mohammed Khamis Abdulla,** Katibu Mkuu na **Nicholaus Merinyo Mkapa**, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, napenda kuwashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kutekeleza majukumu yake imeendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kipekee napenda kushukuru mashirika yafuatayo: Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU); Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU); Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Ubalozi wa Korea Kusini nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nazishukuru pia Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) kwa ushirikiano wao katika masuala ya kikanda na kimataifa yanayohusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea kuchangia katika kutimiza malengo ya Serikali.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, napenda kuwashukuru watoa huduma za mawasiliano kutoka katika makampuni ya simu ya Airtel, Vodacom, Viettel, Honora, TISPA na TTCL kwa utoaji na usambazaji wa huduma za mawasiliano nchini. Napenda pia kuzitambua Taasisi za NMB, CRDB, na TSA kwa mchango wao wa kuendeleza na kukuza bunifu za TEHAMA nchini. Kwa kumalizia natambua mchango wa wadau wote wa Sekta ikiwemo Kampuni ya Minara Tanzania, Herios Tower, Huawei, Softnet, Telecom Associate, TanzTech pamoja na Raddy Fibre.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo zilizopangwa kutekelezwa zinatekelezwa na kuwezesha Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuchangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2026.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho na kwa umuhimu wa kipekee naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu na Taifa kwa Ujumla. Aidha, napenda kumshukuru Mke wangu Bi Mariam Bakari Silaa na familia yangu kwa ujumla pamoja na ndugu, jamaa na marafiki kwa kunipa nguvu na moyo wa kutekeleza majukumu yangu katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26**

**Makadirio ya makusanyo ya maduhuli**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa fedha 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 100,369,242,000** ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**Makadirio ya matumizi**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 291,533,139,000** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na vipaumbele vya Wizara kama ifuatavyo;

**Matumizi ya kawaida**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kutumia **Shilingi 14,485,656,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi **6,958,609,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 7,527,047,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Matumizi ya Miradi ya Maendeleo**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2025/26 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 277,047,483,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 98,480,905,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 178,566,578,000** ni fedha za nje.

18. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni http://www.mawasiliano.go.tz.

19. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.